Mkuranchi – 10 Juni 2010

Wasomi wataka bajeti ya tabasamu

Salim Said

WASOMI nchini wameeleza ku wanatarajia kuwa bajeti itakayosom leo bungeni na Waziri wa Fedha Uchumi, Mustapha Mkulo itakuwa ya tabasamu kwa wananchi na ir lenga kuinua uchumi.

Bajeti zilizopita zililalamikiwa k kutenga mafungu makubwa ya fed katika masuala ya chai za maofisi posho za safari za wakubwa na marup rupu kadhaa ya vigogo wa serikalini.

Wakizungumza na Mwananchi k njia ya simu kwa nyakati tofauti jiji Dar es Salaam jana, wasomi hao amb ni wataalamu katika mambo ya uchu walisema wanataka bajeti ikayoufan uchumi wa Tanzania kusimama i kuimarika na siyo itakayoudidimiza.

Dk Donath Olomi wa Chuo Kik cha Dar es Salaam(UDSM), aliser kwa kuwa nchi imepata pengo kati bajeti yake, baada ya wahisani kuka kusaidia kiasi fulani cha fedha, hiv natarajia kidogo kilichopo kupang kwa vitu muhimu vitakavyopewa k umbele.

"Tunatarajia bajeti ambayo itaten fedha katika vipaumbele vikavyc nyanyua uchumi wetu," alisema Olomi.

Alisema lazima serikali ilenge baj ake katika vipaumbele ambavyo v anye uchumi wa nchi uweze kusimar na kuwacha kuweka nguvu katika narupurupu, chai za maofisini,

1

magari ya kifahari na safari za nje kwa vigogo.

"Bajeti yetu ni ndogo, tusifanye masihara na hizo fedha, tuziweke katika kuinua kilimo kwa kuhakikisha tunawekeza katika ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, bandari na kilimo cha umwagiliaji," alisema Dk Olomi.

Alisema fedha nyingi pia zinapaswa kutengwa katika mafunzo ya kilimo na kuboresha mazingira ya kusoma na kujisomea kwa wanafunzi wa Elimu ya Msingi hadi vyuo vikuu.

"Serikali ihakikishe walimu wapo wa kutosha, maslahi yao yanaboreshwa na mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu itengewe fedha za kutosha ili tuondokane na migomo na maandamano ya mara kwa mara ya wanafunzi," alisema Dk Olomi.

Mwenyekiti Mwenza wa Mpango wa Utafiti wa Elimu ya Demokrasia Tanzania (Redet), Dk Benson Bana alisema wanatarajia bajeti itakayowafanya Watanzania kutabasamu na sio kukasirika.

"Bajeti yetu ya mwaka huu lazima iwafanye Watanzania masikini kutabasamu na sio kukasirika kutokana na machungu ya bajeti hiyo," alisema Dk Bana.

Alifafanua kuwa, "Hii ni bajeti ya uchaguzi, nadhani serikali imejipanga vizuri kusoma bajeti yenye tabasamu kwa kila Mtanzania,".

Alisema bajeti hiyo lazima itowe vipaumbele katika sekta za afya, elimu, miundombinu, kilimo na ulinzi na usalama wa taifa na watu wake.

"Unajua bwana, bajeti ni mchakato wa kisiasa na kila mwanasiasa anajua wananchi wanataka nini kupitia vipaumbele mbalimbali," alifafanua Dk Bana.

Dk Bana alifafanua kuwa, serikali inapaswa kufuta kodi ambazo hazina msingi wowote na kuangalia upya baadhi ya kodi hizo kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kodi ya nyumba na kodi katika mishahara.

"Serikali lazima iangalie kodi hizi za mishahara (pay as you earn) na kodi za nyumba, kwa kweli kodi nyingine ni 'non sense' (hakuna msingi wowote)," alisema Dk Bana na kuongeza;

"Wasiwasi wangu uko zaidi katika vyanzo vyetu vya fedha, kwa sababu hata wahisani naona wameanza kuweka ngumu huku vyanzo vyetu ni vilevile vya sigara na pombe," alisema Dk Bana.

Dk Haji Semboja alisema hakuna jambo jipya litakalotokea katika bajeti ya mwaka isipokuwa ni yaleyale yaliyozoeleka katika bajeti za miaka iliyopita.

Waziri wa Fedha na Uchumi, Mustafa Mkulo akishuka katika gari lake kuelekea bungeni mjini Dodoma jana. Mkulo anatarajiwa kuwasilisha bajeti ya serikali ya mwaka 2010/11 leo. Picha na Edwin Mjwahuzi.

"Kimsingi hakuna kitu kipya katika bajeti ya mwaka huu bali ni yaleyale yaliyozoeleka," alisema Dk Semboja.

"Hofu yangu kubwa ni uamuzi wa wahisani kupunguza misaada yao, lakini, naamini kwamba baada ya uchaguzi wahisani watabadilisha msimamo wao na kuleta fedha, hivyo kutakuwa na 'min budget'(bajeti ndogo)," aliongeza Dk Semboja.

Dk Semboja ambaye pia ni mhadhiri mwandamizi wa masuala ya uchumi UDSM alisema, "Sio kwamba wahisani wamezuia fedha zao kwa sababu ya uchaguzi, bali ni kukosa imani na serikali baada ya mambo mengi waliyoahidiwa kutotekelezwa ipasavyo,".

Hata hivyo, Dk Semboja alisema uchumi wa Tanzania ulikuwa unafanya vizuri kwa miaka miwili ya kwanza katika Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Rais Jakaya Kikwete, lakini uliyumbaa kutokana na mtikisiko wa uchumi wa dunia. "Cha msingi hapa wananchi wasiikasirikie serikali kwa bajeti yoyote ile itakayokuja kwa sababu kila mtu hushona suti kutokana na kitambaa alicho nacho," alisema Dk Semboja.

Alisema vipaumbele vya serikali ni vya gharama sana kwa kuwa vinajumuisha elimu hasa katika shule za kata, polisi kata na zahanati za kata.

"Lakini tatizo kubwa ni kwamba tumeshindwa hadi sasa kuifanya 'productive sector' (sekta ya uzalishaji bidhaa) kuisaidia 'development sector' (sekta ya maendeleo) nchini," Dk Semboja alisema:

"Kwa hiyo lazima tuweke mkazo zaidi katika sekta ya uzalishaji bidhaa na siyo ya kuzalisha huduma na tujitahidi kuweza kudhibiti sekta ya madini ili itumikie uchumi wa taifa,"

Naye Mukrugenzi Mtendaji wa Sikika, Irene Kiria alisema bunge hili la bajeti ni muhimu sa kwa maslahi ya taifa amba wabunge wanapaswa kujadili kupitisha mipango ya serik kwa mwaka ujao.

"Hili ni tukio muhimu m kwa vile linapanga kwa ajili mwaka ujao. Kushindwa kati hatua hii ya kupanga maa yake, tunapanga kushindwa ka ka mwaka ujao," alisema Kiria.

Alisema wabunge wanapasw kuonyesha uaminifu wa kutos kwa Watanzania ili kuhakikis kwamba bajeti hiyo inakuwa kutekelezeka kikamilifu na kw ufanisi kulingana na fedha zi zotengwa.

"Kama kanuni za bunge zin vyoeleza, mbunge anatakiw kupata nakala ya kitabu c bajeti siku 21 kabla ya kus mwa bungeni ili, aweze kuison na kuandaa michango mizu katika kikao cha Bunge. Sij ni wabunge wangapi wamepa nakala hizo," alihoji Kiria.